

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI
[Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)]



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (w)
S.L.P. 20
MISUNGWI.

Simu: 255-732980745

Fax: 255-732980745

BaruaPepe: ded@misungwidc.go.tz

Tovuti: www.misungwidc.go.tz

27/08/2018

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mwenge wa Uhuru mwaka 2018 utapokelewa na kukimbizwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi tarehe **28/08/2018** na utazindua Miradi, kuweka jiwe la Msingi, Kukagua na kufungua miradi ya Maendeleo minane (8) yenye jumla ya gharama ya Shilingi **2,381,277,750/=** .

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Mhe. Juma Sweda ilieleza kwamba Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2018 katika Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi zitafanyika siku ya Jumanne tarehe 28/08/2018, ambapo Mwenge huo utapokelewa katika Kijiji cha Bujingwa Kata ya Fella saa. 2.30 asubuhi ukitokea katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu na utakimbizwa katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Misungwi kwa umbali wa kilomita 108.7 na Mkesha utafanyika katika eneo la Stendi Ndogo ya Usagara.

Amesema kwamba Mwenge wa Uhuru katika Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi utapita katika miradi mbalimbali ambayo ni Kiwanda cha Gesi ya Majumbani cha Usagara chenye gharama ya Shilingi 790,000,000, Matengenezo ya mtandao wa barabara ya Misungwi mjini yenye Shilingi 42,682,500, Mradi wa Bwawa la Samaki Sawenge wenye Shilingi 154,700,000, Mradi wa uhifadhi wa Maji na kisima Mitindo wenye Shilingi 68,797,000/=

Amebainisha Miradi mingine ni pamoja na Mradi wa ujenzi wa Jengo la Kitengo cha Bima ya Afya Hospitali ya wilaya lenye thamani ya Shilingi 141,525,250, Mradi wa Shule ya Sekondari ELPAS kwa gharama ya Shilingi 1,020,000,000, Shughuli ya Utoaji wa Mikopo kwa Vijana, Wanawake na Walemavu Shilingi 50,000,000 na Mradi wa Maabara ya Kompyuta wa Mitindo wenye gharama ya Shilingi 113,573,000. Aidha, fedha hizo zinatokana na mchango wa Halmashauri ambazo ni shilingi 196,625,250, mchango wa Serikali kuu kiasi cha shilingi 106,282,500 pamoja na fedha za michango ya Wahisani kiasi cha shilingi 2,078,370,000.

Mkuu wa Wilaya ya Misungwi ameeleza kuwa **ujumbe Mkuu wa mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2018 ni "Elimu ni ufunguo wa maisha Wekeza sasa kwa maendeleo ya taifa letu"** na amewataka Wananchi wote wa Wilaya ya Misungwi kujitokeza kwa wingi kuupokea, kuushangilia kwa furaha wakati wote na katika maeneo yote utakapopita kwa ajili ya kukagua, kufungua na kuweka jiwe la Msingi kwenye miradi husika na kwamba Mwenge wa Uhuru ni ishara ya amani, upendo na umoja pia ni kichocheo cha maendeleo kwa Wananchi.

Kwa Mujibu wa taarifa hiyo ya Mkuu wa Wilaya ya Misungwi inaeleza kwamba, Mwenge wa Uhuru utakabidhiwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Sengerema siku ya Jumatano saa 1.30 asubuhi tarehe **29/08/2018** katika Kijiji cha Busisi kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.



Thomas Lutego

KAIMU MKUU WA KITENGO CHA TEHAMA NA UHUSIANO (W)
MISUNGWI

27 Agosti, 2018